# KWA NINI SIENDI KANISANI TENA?

**Na Wayne Jacobsen**

**Kwa mwamini mwenzangu,**

Ninatambua jinsi unavyo nijali na hiyari yako ya kunijulisha mambo ambayo yamekujalisha . Ninajua kwamba jinsi ninavyohusiana na kanisa sio sawa na vile wengi wamezoea na wengine hata husema ya kwamba ni hatari. Niamini, ninajua kujali kwako kwa sababu nilikuwa nikiwaza hivyo na hata nilifundisha watu wengine kuwaza hivyo.

Kama wewe umetosheka na hali ya mpangilio wa dini leo, huenda usipende yale unasoma hapa. Makusudi yangu sio kukushawishi wewe kuona kanisa jinsi ninaona lakini kujibu maswali yako kwa njia iliyo wazi niwezavyo.

Hata tusipokubaliana, ninatumaini kwamba utaelewa ya kwamba tofauti zetu hazistahili kututenga sisi kama sehemu ya mwili wa Kristo.

**Unaenda wapi kanisani?**

Sijawai penda hili swali hata wakati nilipoweza kujibu ni ushirika fulani. Ninajua maana yake kidesturi lakini imejengwa kwa msingi mbaya ya kwamba kanisa ni kitu unayoweza kwenda kama kwa sherehe maalum, mahali fulani au kikundi kilicho na mpangilio. Ninafikiri kwamba Yesu anatazama kanisa vitofauti kidogo. Yeye hakusema kwamba ni mahali pa kwenda , lakini ni jinsi ya kuishi kwa uhusiano na yeye na wanfunzi wake wengine.

Kuniuliza ninaenda wapi kanisani ni sawa na kuniuliza ni wapi ninaenda kwa Jacobsen. Nitajibu swali hiyo vipi? Mimi ni Mjacobsen na pale ninapokwenda Mjacobsen yuko hapo “kanisa” ni neno kama hilo. Haielezi kuwa ni mahali fulani au ushirika fulani. Inaeleza kuwa ni watu Fulani na jinsi wanovyoshirikiana. Tukipoteza maono hayo, ufahamu wetu kuhusu kanisa itakuwa mbaya na tutakosa furaha ya kanisa.

**Unajaribu kuepuka hii swali?**

Ninajua inaweza kusikika kama kusema maneno mengi tu, lakini maneno ni muhimu. Tukisema neno kanisa linamaanisha kusanyiko la mwisho wa juma au mashirika yaliyojipanga kama makanisa tunakosea maana ya kuishi kama mwili wa Kristo. Inatupatia hali ya usalama wa uongo kuwaza kwamba kwa kuenda kwa mkutano mara moja kwa juma basi sisi tunajihusisha katika  kanisa la Mungu.Mara nyingi ninasikia watu wakiongea juu ya 'kuacha kanisa' wakati wanaacha kuhudhuria kusanyiko fulani.

Lakini kama sisi ni kanisa, wala sio mahali tunakwenda, twawezaje kuicha ijapokuwa kumwacha Yesu mwenyewe?  Na kama mimi ninafikiri kuwa kusanyiko fulani ndilo kanisa, je sinimejitenga na ndugu na dada wengine wasioenda mahali ninapokwenda.

Hilo wazo kwamba watu wanaokusanyika jumapili asubuhi kutazama waimbaji sifa na kusikiliza mafundisho ni sehemu ya kanisa na wale wasiokusasnyika sio kanisa ni jambo mgeni kwa Kristo.  Swala sio mahali tulipo wakati fulani wa mwisho wa juma, lakini ni jinsi gani tunaishi ndani ya Kristo na jinsi tunavyoishi na waamini wengine katika juma lote.

**Lakini si tunahitaji ushirika kila wakati?**

Singesema tunahitaji. Kama tungelikuwa mahali penye hatungepata waamini wengi, hakika Yesu angeweza kutulinda. Wacha niseme maneno haya kwa njia tofauti: watu wanaokuwa kwa kumjua Mungu aliye hai watatamani uhusiano na waaminio wengine. Bila shaka, mwito kwa ufalme wa Mungu sio mwito wa kujitenga.  Kila mtu niliekutana naye anayefaulu katika maisha ya Kristo anatamani kuwa na waaminio wengine. Wanatambua kwamba chochote wanajua kuhusu maisha ya Mungu ni sehemu kidogo tu na ufunuo kamili wa Mungu uko kanisani.

Lakini mara nyingi ushirika wa aina hiyo sio rahisi kuipata.  Wakati mwingine katika safari hii tunapitia wakati ambapo hatupati waumini wengine walio na njaa kama sisi. Hiyo haswa ni kweli kwa watu ambao wanapata kwamba kufuatia matarajio ya dini zinazowazingira inadunisha uhusiano wao na Kristo.  Wanaweza kujipata wametengwa na waumini wengine ambao wamekuwa marafiki wa karibu.  Lakini hakuna mtu

anayepitia hali kama hiyo huona kuwa ni nzuri. Ni hali ya uchungu sana wao watatafuta waumini wengine walio na njaa kushiriki nao hiyo safari.

Maelezo inayonipendeza kuhusu maisha ya mwili ni mahali pale kikundi cha watu kinachagua kutembea pamoja kwa sehemu fulani ya safari kwa kutengeneza urafiki wa karibu na kujifunza kusikia sauti ya Mungu pamoja.

**Twapaswa kujitolea kwa ushirika Fulani?**

Hio imenenwa mara nyingi leo mpaka wengi wetu wanafikiria kuwa iko kwa bibilia mahali fulani. Sijawai ipata bado. Wengi wetu tumefanywa kuamini kwamba hatuwezi kufaulu pasipo kuwa na ‘ufuniko wa mwili’ na ya kwamba tutaanguka kwa upotovu au kurudi nyuma kwa dhambi. Lakini jambo hilo linatendeka katika kusanyiko

Ninajua watu wengi wanaoishi inje ya mipangilio kama hiyo na wanapata sio tu uhusiano unaoendelea na Mungu na uhusuiano na waumini wengine wanaotaka uhusiano wa ndani kuliko uliokuwa katika kusanyiko. Sijawai poteza moto wa kumfuata Yesu au upendo wangu kwa kanisa lake. Kama kuna jambo ni kwamba mambo hayo yamekuwa sana kwa miaka michache iliyopita

Maandiko inatuhimiza tujitolee sisi kwa sisi na wala sio kujitolea kwa ushirika fulani. Yesu alieleza kwamba popote watu wawili au watatu wanakusayika wakimwelekea yeye, basi wao watafurahia uzuri wa maisha ya kanisa.

Je inasaidia kuhusika mara kwa mara kwa kudhihirisha ukweli huo? Bila shaka ndiyo. Lakini tunafanya makosa kufikiria kuwa ushirika unakuweko kwa sababu tunahudhuria ibada, mara kwa mara, au kwa sababu tuko kwa ushirika moja. Ushirika unatendeka mahali ambapo watu wanashiriki safari ya kumjua Yesu pamoja .Inahushisha kushiriki mambo yetu wazi ,kujali kwa kweli kuhusu kukuwa kwa kila mmoja wetu kiroho na kuhimiza watu kumfuata Yesu jinsi anavyowaongoza.

**Lakini ushirika zetu zinatulinda na kupotoka?**

Pole sana kwa kupasua kidogo hapa lakini uongo wote uliyowekwa juu ya watu wa Mungu kwa miaka elfu mbili iliyopita umetokana kwa vikundi vilivyokuwa na mpangilio na 'viongozi' ambao walifikiri kuwa walijua nia ya Mungu kuliko mtu yeyote mwingine aliyekaribu nao. Kila utembezi wa Mungu kati ya watu walio kuwa na nja ya Mungu ilikataliwa na 'kanisa' ya siku hiyo na walitengwa na kufukuzwa au kuuwawa kwa kumfuata Mungu.

Kama hapo ndio unatumaini kupata usalama ninahofu umepotoka .Yesu hakutueleza kwamba kwa kuenda kanisani itatuweka salama lakini kumuamini yeye ndio itatuweka salama. Yeye alitupa upako wa Roho mtakatifu ili tuweze kujua tofauti ya ukweli na uongo. Upako huo unachochewa na kukuzwa tunapojifunza njia zake kwa neno lake na kukaribia moyo wake.. Itakusaidia wewe kutambua wakati kanisa unaloshirika maisha nayo inakuwa ya uharibifu kwa kazi yake ndani mwako.

**Kwa hivyo kusanyiko ni mbaya?**

La hasha! Nimepata nyingi ya hizo ushirika na watu wanaopenda Mungu na wanatamani kukuwa katika njia zake. Ninatembelea shirika kadha katika mwaka ambayo ninapata yanahusika na uhusiano na sio dini tu. Yesu yuko katikati ya maisha yao pamoja na wale ambao ni viongozi ni watumishi wa kweli na hawachezi siasa ya uongozi. Kwa hivyo hii inatia changamoto watu kuhudumiana wao kwa wao.

Ninaomba kwamba wengi wao wanahuishwa kuwa na bidii ya kumfuata Yesu, kumaanisha kujali wao kwa wao na kuwa na hiyari ya kutumikia ulimwengu na upendo wa Mungu.

Lakini ninafikiri tutakubali kwamba haya ni kidogo sana katika jamii zetu na nyingi zinadumu kwa muda mfupi kabla hazijaanza kutafuta suluhisho kwa mashirika kwa mahitaji ya mwili pasipo kuishi kumtegemea Yesu. Hiyo ikitendeka usihukumike kama Mungu atakuongoza kutokwenda pamoja nao.

**Kwa Hivyo Niaache Kwenda Kanisani Pia?**

Hiyo swali imekosa mwelekeo. Mimi siamini kwamba wewe unaenda kanisani zaidi yangu. Sisi tu sehemu ya hiyo,kuwa sehemu yako jinsi Yesu anavyokuita na popote anapokuweka.Sio sisi wote tunakuwa kwa mazingira sawa.

Kama wewe unakusanyika na waumini wakati fulani na mahali fulani na hiyo inakufanya wewe kukuwa karibu na Yesu na inakuwezesha kufuata kazi yake ndani yako, kwa njia zote sidhani kuwa unastahili kutoka .Lakini ujue kwamba hiyo peke yake sio kanisa. Ni moja ya dhihirisho ya kanisa mahali unapoishi.

Usidanganyike kwamba kwa sababu unahudhuria mikutano yake basi wewe unapokea maisha ya kweli ya mwili. Hio inakuja tu wakati Mungu anakuunganisha na wandugu na wadada wachahce ambao unaweza kujenga urafiki wa karibu na kushiriki milima na mabonde ya safari hii ya wokovu.

Hiyo inaweza kutendeka katika ushirika zinazojulikana na hata inaweza kutenda zaidi ya hizo ushirika.Kwa miaka saba iliyopita nimekutana na mamia na maelfu ya watu waliochoka na desturi ya kusanyiko na wanaendelea vyema kiroho wanaposhiriki maisha ya Mungu na watu wengine manyumbani mwao.

**Kwa hivyo kukutana manyumbani ndio jibu?**

La hasha. Tuwe wazi jinsi inavyopendeza kufurahia ushirika mkubwa wa kuabudu na kufundishwa  na wa walimu walio na kipawa, furaha ya ukweli wa mwili hauwezi kuushiriki kwa vikundi vikubwa .Kanisa kwa miaka yake mia tatu ya kwanza ilipata nyumbani kuwa mahali sawa kukusanyika. Nyumbani inafaa sana hali ya jamii na hivyo ndivyo Yesu alielezea mwili wake kuwa.

Lakini kukutana manyumbani sio tiba ya yote. Nimewahi kuwa katika ushirika za nyumbani ambazo ni mgonjwa na pia nimeenda kwa ushirika mkubwa ulioshiriki maisha ya mwili pamoja. Lakini wakati ninoakuwa muda kwa muda ninataka nishiriki ana kwa ana na kikundi cha watu. Ninajua sio jambo la kawaida leo hii mahali ambapo watu wanaipata rahisi kuketi katika ibaada iliyopangwa vizuri (au ikupangwa vizuri) na kwenda nyumbani pasipo kufunua maisha yao au kujali safari ya mtu mwingine.

Lakini hatimaye kinachojalisha kwangu mimi sio wapi au vipi wanavyokutana lakini iwapo watu wamemwelekea Yesu na wanasaidiana kwa ukweli kwa safari hii ya kukuwa

na kufanana kama Yesu.Mikutano sio muhimu hapa kuliko hali ya uhusiano. Kila wakati ninatafuta watu kama hao mahali popote nilipo na kila wakati ninafurahi ninapoipata. Nyumbani kwetu Moorpark tumewapata marafiki wachache na tunatumaini kupata hata wengine.

**Wewe unaitikia kutokana na kuumizwa?**

Ndivyo inawezekana na wakati utatueleza, ninafikiri lakini kwa wazi siamini ni hivyo. Kila mtu anayehusika katika maisha ya mwili ya kweli ataumia wakati mwingine. Lakini kunakuumia aina mbili kuna ule uchungu unaokuelekeza kwa shida inayoweza kutatuliwa kwa kujali sawa -kwa mfano kuteguka kwa mguu. Alafu kuna ule uchungu unaoweza kuregebishwa kwa kuondoa kitu- kwa unapoweka mkono juu ya moto.
Labda kila moja wetu amepitia kiwango fulani ya uchungu tunapojaribu kuweka maisha ya Mungu kwa mashirika.Mara nyingi wengi wetu tunaketi pale tukitumaini kwamba tukifanyiwa mambo fulani basi hali itakuwa bora zaidi.Ndio tunaweza kufaulu kwa kiasi fulani wakati wa huiisho tulitambua kuwa hatimaye ya kwamba kufuata masharti ya mashirika na uhuru watu wanahitaji kuwa katika Kristo yako mbali mmoja na nyingine. Imetendeka na karibu kila kikundi iliyoundwa katika historia yote ya Uskristo.

**Unatafuta kanisa iliyo kamilifu?**

La na sitazamii kupata moja upande huu wa umilele.Ukamilifu sio lengo langu lakini kupata watu walio na mambo yanayo mpendeza Mungu. Ni jambo moja watu kuweka bidii kuelekea jambo wanaloliamini na ni jambo lingine kutambua kwamba mambo tunayoamini yana mambo machache sana yaliyo sawa. Sifanyi siri yoyote kwamba ninasumbuliwa sana na Ukristo wa mpangilio. Mengi ya yale tunaita 'kanisa' leo si kitu zaidi ya mipango iliyopangwa vyema pasipo kuwa na uhusiano kati ya waaminoi .Waumini wanaelekezwa kuweka tumaini lao kwa mipangilio na uongozi na sio kwa Kristo mwenyewe. Tunatumia muda mwingi kufuatisha watu mambo ambayo ushirika unataka badala ya kusaidia watu wageuzwe chini ya msalaba wa Yesu.
Nimechoka kushiriki na watu ambao wanaona kanisa kuwa mahali ambapo wanakuja kwa masaa mawili kwa juma kupata hukumu zao na kisha wanaishi juma lote lingine wakifuatisha mambo ya ulimwengu. Nimechoka na watu wanotegemea kazi zao za haki

lakini hawana upendo kwa watu wa ulimwengu.  Nimechoka na watu ambao wana uogi na wanatumia mwili wa Kristo kueneza ubinafsi wao na wataidanganya kutosheleza mahitaji ya ubinafsi.  Nimechoka na mahubiri yaliyojaa utumwa wa dini kuliko uhuru wa upendo wa Mungu na mahali ambapo uhusiano unawekwa nyuma kwa masharti ya shirika.

**Lakini si watoto wetu wanahitaji mpangilio wa kanisa?**

Ningesema kwamba kile wanachohitaji zaidi ni kuingishwa kwa maisha ya Mungu kupitia ushirika wa uhusiano na waumini wengine.  Asili mia tisaine na mbili (92%) ya watoto wanaokuwa katika shule ya Jumapili na vinyago na kuburudishwa, wanatoka 'kanisa' wanapotoka nyumba za wazazi wao.  Badala ya kujaza watoto wetu na tabia na sheria tunahitaji kuwaonyesha jinsi ya kuishi katika maisha ya Mungu pamoja.

Hata wanasociologia wanatuambia kwamba jambo la kwanza litakalothibitisha kama mtoto ataishi vyema katika jamii ni kama wana urafiki wa ndani na wa karibu na watu wengine wakubwa ambao sio wa jamii ya karibu nao.  Hakuna shule ya jumapili inaweza kujaza hiyo pengo.  Ninajua kuhusu jamii moja kule Australia ambayo baada ya miaka ishirini ya kushiriki neno la Mungu pamoja kama jamii mbali mbali wangesema kwamba hawajawahi kumpoteza hata mtoto mmoja kwa imani ya Kristo walipokuwa watu wakubwa.  Ninajua nimeenda kinyume hapa lakini ni muhimu ya kwamba watoto wetu wawe na ushirika ya ukweli kati ya waumini kuliko kuwa na kengele na firimbi ya mpangilio mzuri ya watoto

**Unatafuta nini kwa maisha ya mwili?**

Kila wakati ninatafuta watu ambao wanatafuta kumfuata kristo aliye hai.Yeye yuko katikati ya maisha yao, upendo wao na mazungumzo yao wanataka wawe wazi na kuwacha watu wawe uhuru kuumia wakati wanaumia, kuuliza yale wanaulizia na kufuata sauti yake pasipo pengine kuwashtaki kuleta migawanyiko au kuasi.  Ninatafuta watu ambao hawapotezi pesa zao kwa mijengo ya bei kali au mipangilio; mahali ambapo  watu wakikaa pamoja wao sio wageni, na mahali ambapo wote wanahusika kama makuhani kwa Mungu badala ya kutazama pasipo kuhusika kutoka mbali.

**Si unapatia  watu sababu ya kuketi nyumbani pasipo kufanya kitu?**

Na tumaini la, ijapo ninajua kuwa ni hatari.  Nimetambua kuwa watu wengine wanaoacha mashirika yao wanatumia vibaya uhuru huo kushibisha tama zao wenyewe na kwa hivyo wanakosa maisha ya kanisa. Wala mkimi sifurahii 'waruka makanisa' wanaotoka mahali pamoja hadi pengine wakitafuta mambo mapya na nafasi bora kutimiza tama zao.

Lakini watu wengi ninaokutana nao na kuongea nao hawako inje ya mpangilio kwa sababu wamepoteza hamu ya Yesu na watu wake, lakini kwa sababu mashirika yaliyo karibu nao yangeshibisha njaa yao ya uhusiano wanatafuta dhihirisho ya maisha ya mwili na wanalipa gharama kubwa kuitafuta.  Niamini mimi, tungeipata wote rahisi kwenda na mtiririko lakini ukishaonja ushirika uliyohai kati ya waumini walio na hamu,ni vigumu kutaka kitu kingine chini ya hiyo.

**Maono haya ya kanisa sio ya kuleta migawanyiko?**

Sio hivyo.Watu wanafanya kugawanya wakati wanataka watu wafuate ufunuo wao wa ukweli.  Wengi wetu katika safari hii twashtakiwa kuwa na mgawanyiko kwa sababu uhuru unaweza kuwa tishio Kwa watu wanaopata usalama wao kwa mpangilio wa kidini lakini wengi wetu hatutakii kuwasajili watu kuacha mashirika yao.Tunaona mwili wa Kristo kuwa kubwa ya kutosha watu wote wa Mungu lakini Mungu anawewahitaji watu wake wakusanyike.

Jambo moja linalosemwa kuhusu kanisa ni kwamba jumapili asubuhi ndiyo masaa iliyotengwa katika desturi ya Marekani. Tunakutana tu na watu wanaofanana jinsi tunavyofanana na wanapenda vitu jinsi tunavyopenda. Nimetambua sasa kwamba ninayo nafasi kukutana na watu kutoka kwa sehemu pana ya mwili wake. Siamurishi watu jinsi ninavyofanya na ninatumaini kwa wakati kwamba wao wanaoiona vitofauti wataacha kutuamuru kufuata yao.

**<u>Nitapata wapi ushirika huo?</u>**

Hakuna jibu rahisi hapa.Inaweza kuwa wazi mbele yako katika ushirika uliyoko sasa hivi. Inaweza kuwa barabarani kwa majirani au mahali pa kazi. Unaweza pia kuhusika kwa

huduma ya upendo kuwafikia walio na mahitaji na waliofanyika mahali unapoishi kama njia ya kuishi maisha yake ndani yako na kukutana na wengine walio na njaa kama hiyo. Usitarajie aina ya ushirika hii kukuwa shiriki kwa urahisi. Yesu anaweza kukuongoza mahali ulipo sasa. Mtafute kuweka watu kadha katika maisha yako ambao mnaweza kushiriki safari.Labda wote hawataenda kwa ushirika sawa na wewe. Wanaweza kuwa majirani au wafanyakazi wenzako ambao wanamtafuta Mungu. Je kuunganishwa kama huo kati ya watu wa Mungu hautazaa matunda ya ajabu.

Usitarajie iwe rahisi au iende sambamba.Itatugharimu kufanya uamuzi kwa upande wetu kumtii Yesu. Itagarimu mazoezi fulani kutingiza tabia fulani na wewe kuwa huru kumwacha yeye kujenga jamii yako.Kandoyaako, lakini inastahili. Ninajua inasumbua watu fulani ya kwamba sichukuinafasi yangu ya kawaida kwa madhabahu ya kanisa Jumapili, lakini ninaweza kukuambia kwamba siku zangu mbovu inje ya dini ya mpangilio ni bora kuliko siku bora ndani ya dini ya mpangilio.Kwangu mimi tofauti ni kama kumsikiliza mtu kuongea juu ya kucheza mpira au kuchukua mpira na kwenda uwanjani na kucheza. Kwa kanisa lake ni hivyo.Kwa siku zetu hizi hatuhitaji mazungumzo mengi juu ya kanisa, lakini watu ambao wako tayari kuishi ukweli wa kanisa.

Watu ulimwenguni kwote kwa upya wanatambua jinsi ya kufanya hivyo tena.Unaweza kuwa mmoja wao unapomuacha akuweke katika mwili wake jinsi apendavyo.